**BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA UCHUMI NA UWEKEZAJI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA VIJANA, AJIRA NA UWEZESHAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

*[Imetolewa kwa mujibu wa Kanuni 124 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Zanzibar Toleo la Februari, 2024]*

**June, 2026**

## 1.0 SEHEMU YA KWANZA

## 1.1 UTANGULIZI

Awali ya yote, napenda kutanguliza shukurani zangu za dhati kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu mwingi wa Rehma mwenye kurehemu kwa kutujaalia afya na uzima . Namuomba Allah Mtukufu azidi kutukirimu neema zake ambazo kwa hakika sote ni wahitaji kwake.

**Mheshimiwa Spika,** tunamshukuru pia Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dr. Hussein Ali Mwinyi kwa uongozi wake imara na thabiti unaowaletea maendeleo ya haraka wananchi wa Zanzibar.

**Aidha,** naomba pia kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zanzibar kwa uongozi, hekima, busara na uweledi katika kuliendesha Baraza hili Tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Baraza ya Uchumi na Uwekezaji ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umetuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi .Naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu za Hansard ya Baraza kama yalivyo wasilishwa katika taarifa hii; nayo ni kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| i. | Mhe. Makame Mohammed Sufiani | Mwenyekiti |
| ii. | Mhe Dr. Mahmoud Omar Mohammed | M/Mwenyekiti |
| iii. | Mhe. Alley Masoud Alley | Mjumbe |
| iv. | Mhe. Shafi Mohammed Shafi | Mjumbe |
| v. | Mhe. Chumu Kombo Khamis | Mjumbe |
| vi. | Mhe. Tabia Maulid Mwita | Mjumbe |
| vii. | Mhe. Toufiq Salim Turky | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| viii. | Ndg. Talib Enzi Talib | Katibu |
| ix. | Ndg. Abdu Maulid Haji | Katibu |
| x. | Ndg. Shaaban Suleiman Juma | Katibu Bajeti |

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Waziri na Naibu Waziri wa Vijana,Ajira na Uwezeshaji kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara yake kwa ufanisi. Aidha, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri wanayofanya kumsaidia Mheshimiwa Waziri.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 124(1) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Zanzibar, Toleo la Februari, 2024, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Uchumi na Uwekezaji ya Baraza la Wawakilishi, Zanzibar kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Vijana,Ajira na Uwezeshaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 124(2) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Zanzibar, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

**i.** Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi pamoja na kuelezea misingi iliyotumika katika uandaaji wa Taarifa hii pamoja na namna Kamati ya Uchumi na Uwekezaji ilivyofanya kazi;

**ii.** Sehemu ya Pili ni ya uchambuzi wa kina juu ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Kazi na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

iii. Sehemu ya Tatu ni uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027;
iv. Sehemu ya Nne ni maoni pamoja na ushauri wa Kamati na
v. Sehemu ya Tano ni hitimisho.

## 1.2 Msingi wa Uchambuaji wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa uchambuaji wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji unatokana na matakwa ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Zanzibar, 2024. Kanuni ya 119(3) zinaipa Kamati hii miongoni mwa majukumu mengine, jukumu la kufanya uchambuzi wa Bajeti na Makadirio ya Wizara hii.

Aidha, Kanuni ya 101 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Zanzibar Toleo la mwaka 2024 imeweka masharti yanayoelekeza kuwa Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Wizara hii kuchambuliwa na Kamati ya Uchumi na Uwekezaji kabla ya kujadiliwa Baraza la Wawakilishi, Zanzibar.

Hivyo, naomba kulijulisha Baraza lako tukufu kuwa masharti hayo yaliyoelekezwa katika Kanuni zetu za Baraza yamezingatiwa na kwamba naliomba Baraza lako Tukufu liijadili hoja ya Wizara ya Vijana,Ajira na Uwezeshaji pamoja na Taarifa hii ya Kamati ya Uchumi na Uwekezaji.

## 1.3 Maeneo ya Uchambuzi wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Wizara ya Vijana,Ajira na Uwezeshaji inagusa mafungu mawili: Fungu **055** (**Vijana, Ajira na Uwezeshaji**) na Fungu **105 (Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi)**

**Mheshimiwa Spika,** aidha Wizara katika mwaka wa fedha 2026/2027 itaendelea kutekeleza Mipango yake kupitia Programu Kuu tatu (3) na

Programu ndogo 7 ambazo ni;

i. Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu **(P01)**
ii. Programu Kuu ya Maendeleo ya Vijana **(P02)**
iii. Programu Kuu ya Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha na Maendeleo ya Ushirika **(P03)**

Naomba kutoa taarifa mbele ya Baraza lako Tukufu kuwa, Kamati ilichambua taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Programu zote tatu pamoja na Programu ndogo zilizoambatana na Programu Kuu.

## 2.0 TAARIFA YA UCHAMBUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA WIZARA YA VIJANA, AJIRA NA UWEZESHAJIKWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi unaweka misingi ya Kikanuni kwa Kamati hii kutoa ushauri unaohusiana na Hoja hii ya Wizara ya Vijana,Ajira na Uwezeshaji . Uchambuzi wetu ulijielekeza katika maeneo makuu manne yafuatayo; -

i. Makusanyo ya mapato;
ii. Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti kwa mwaka wa fedha unaoishia 2025/2026;
iii. Muelekeo wa Wizara katika bajeti ya 2026/2027; na
iv. Utekelezaji wa maagizo ya Kamati.

### 2.2 Uchambuzi wa Makusanyo ya Mapato

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Vijana,Ajira na Uwezeshaji ilipangiwa kukusanya Shilingi **647,000,000** kati ya hizo Shilingi **550,000,000 Unguja** na **Shilingi 97,000,000** Pemba kutoka katika vyanzo vyake vya mapato. Hadi kufikia Machi 2026, Wizara imefanikiwa kukusanya Shilingi **189,638,000** sawa na asilimia **38.**

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi wa Kamati kuhusu makadirio hayo ya Wizara kwa mwaka wa fedha unaoelekea kumalizika, umebaini kuwa mwenendo wa ukusanyaji wa mapato hayo haukuwa mzuri ukizingatia makusanyo ya jumla yaliyokadiriwa .

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa mwenendo huo usioridhisha wa makusanyanyo kwa baadhi ya vyanzo vya Wizara hii ikiwemo idara ya Ushirika unatokana na kukosekana kwa muendelezo wa taarifa za mapato kwa mwaka huu wa fedha 2025/2026 kati ya Wizara ya Kazi na Uwekezaji ambapo Idara ya Ushirika ilikua chini ya Wizara hiyo na Wizara ya Vijana Ajira na Uwezeshaji ambapo kwasasa Idara hiyo imehamishiwa chini yake.

## 2.3 Uchambuzi wa Matumizi ya Wizara

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ilikadiriwa kutumia **Shilingi 20,419,108,690** kati ya fedha hizo **Shilingi 1,133,095,000** mshahara, **Shilingi 2,786,013,690** matumizi ya kazi za kawaida na **Shilingi 16,500,000,000** ni kazi za Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, Wizara imeingiziwa **Shilingi 4,575,140,175** sawa na asilimia **30.** Kati ya hizo **Shilingi 754,627,447** sawa na asilimia **89** mshahara**, Shilingi 1,628,123,428** sawa na asilimia **77** matumizi ya kazi za kawaida na **Shilingi 2,192,389,300** sawa na asilimia **18**

kazi za Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati kuhusu upatikanaji huo wa fedha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Wizara na kazi za maendeleo kwa kweli hauridhishi kwa mwaka wa fedha 2025/2026, hasa ukizingatia katika kufikia malengo ya jumla ya Serikali ya kuwaendeleza Vijana nchini. **Mheshimiwa Spika,** asilimia ya fedha iliyopatikana kwa kazi za kawaida na za maendeleo ni ndogo mno katika kuiwezesha wizara kutekeleza shughuli zake .

**Mheshimiwa Spika,** Hivyo, ushauri wa Kamati hii kuiomba Serikali katika kipindi hiki kilichobaki kuiwezesha vyema Wizara ili kukamilisha na kuyafikia malengo yaliyopangwa mwaka huu wa fedha 2026/2027.

## 2.4 Uchambuzi wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Vijana Ajira na Uwezeshaji, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ilikadiriwa kutumia Shilingi 16,500,000,000 kwa ajili ya kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2026, Wizara imeingiziwa Shilingi 2,192,389,300 sawa na asilimia 18 kwa ajili ya kazi za Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Tathmini ya Kamati katika upatikanaji wa fedha kwa kazi za maendeleo kwa mwaka wa fedha unaoisha bado ni asilimia ndogo hivyo mazingatio yanahitajika ili kufanikisha utekelezaji wa mipango ya Miradi ya maendeleo ya Wizara.

## 2.5 UTEKELEZAJI WA MAELEKEZO YA KAMATI

Kamati inaishukuru Wizara ya Vijana,Ajira na Uwezeshaji kwa kuendelea kutekeleza maelekezo ya Kamati .Kamati yetu ya Uchumi na Uwekezaji imeridhika na ufanyaji kazi wa Wizara katika kutekeleza Sera ya Serikali katika kuwaendeleza Vijana na

kuwainua kiuuchumi.

## 3.0 MAPITIO YA MATUMIZI NA MAPATO KWA FUNGU LA WIZARA YA VIJANA, AJIRA NA UWEKEZAJI (055) KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

### MATUMIZI

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, **Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji fungu 055** imeomba kuidhinishiwa Shilingi **19,050,239,024** kati ya fedha hizo, **Shilingi 3,500,000,000** kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi 4,321,087,100** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, kati ya hizo **Shilingi 3,940,000,000** kutoka Serikalini na **Shilingi 381,087,100** kutoka kwa Washirika wa Maenedeleo, **Shilingi 1,229,151,924** Ruzuku kwa Baraza la Vijana na **Shilingi 10,000,000,000** kwa kutekeleza kazi za Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha **Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Fungu 105,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 **Shilingi 52,850,532,000** zitahitajika kutekeleza mpango kazi wa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,486,340,000** Mishahara, **Shilingi 3,064,192,000** Matumizi Mengineyo na **Shilingi 47,300,000,000** kwa ajili ya kazi za Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kupungua kwa makadirio ya matumizi yaliyopangwa katika mwaka mpya wa fedha wa 2026/2027 kutoka **Shilingi 20,419,108,690** ya makadirio ya mwaka wa fedha 2025/2026 hadi kufikia shilingi **19,050,239,024** kwa mwaka wa fedha 2026/2027.Kamati imeelezwa kuwa miongozi mwa sababu ya kupungua

kwa makadirio hayo ni kupungua kwa vyanzo vya mapato.

## MAPATO

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji **Fungu 055** inakadiriwa kukusanya Shilingi **100,000,000** ikiwa ni mapato ya Usajili na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika. Kamati imebaini kuwa makadirio hayo yamepungua ukilinganisha ya mwaka wa fedha unaomaliza 2025/2026 kutoka shilingi 647,000,000 hadi kufikia shilingi 100,000,000 ambapo hali hiyo imetokana na hali halisi ya makusanyo na Wizara kubakia na chanzo kimoja tu cha makusanyo yatokanayo na Idara ya ushirika.

## 4.0 MAONI YA JUMLA YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia uchambuzi kuhusu Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Kamati hii inatoa maoni ,ushauri na mapendekezo ya jumla kwa mafungu na Programu zote kama ifuatavyo:

1. Kamati inampongeza Dkt, Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la mapinduzi kwa kuunda Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji nchini . Kuwepo kwa Wizara hii kutasaidia kutatua changamoto za Kazi na Ajira zinazokabili maendeleo ya vijana.

2. Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar umeweka mikakati madhubuti ya kujenga mazingira rafiki na wezeshi kwa maendeleo na ustawi kwa vijana ambapo miongoni mwa mikakati hiyo ni kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kutoka asilimia 19 kwa mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 10 kwa mwaka 2025. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kutoa takwimu halisi juu ya hali iliyofikiwa hivi sasa kuhusu matokeo ya mkakati huo ili jamii iweze kufahamu juhudi za serikali katika kukabiliana na suala la ajira kwa vijana.

3. Kamati inaishauri Wizara kuwa na Mpango mkakati wa muda mrefu wa kufanya tafiti mbali mbali kuhusu changamoto zinazowakabili Vijana nchini.

4. Kamati inaishauri Serikali ifanye mabadiliko ya Sera ya Vijana kwani Sera hiyo ni ya zamani ili iweze kuendana na wakati.

5. Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa inasimamia ipasavyo changamoto zilizopo katika taratibu za kusajili vikundi vya Ushirika ikiwemo uhaba wa maofisa wa Ushirika katika Wilaya ili kuona kuwa vikundi hivyo vinaendesha shughuli zake kwa mujibu wa Sheria.

6. Kamati inaishauri Wizara kuharakisha kuanzisha Mfumo maalum utakaotumika katika kufanya uhakiki wa marejesho ya mikopo kutoka kwa wadau wanaopatiwa huduma hiyo.

7. Aidha, Kamati inaishauri Wizara kuharakisha kuanzishwa Mfumo wa Ajira kwa Vijana ili kuwawezesha Waajiri kujisajili na kutambilika rasmi.

8. Kamati inaishauri Wizara kuongeza nguvu katika utoaji wa elimu kwa Vijana juu ya kufanya kazi katika sekta binafsi na fursa zake.

9. Kamati inaishauri Wizara kuendelea kuwashajihisha vijana kujiunga na mabaraza ya vijana hasa katika ngazi za chini, sambamba na kuyaimarisha katika sekta ya elimu na Uchumi.

10. **Kamati inaishauri Wizara kuyaimarisha mabaraza ya vijana**

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho, napenda kuwashukuru na kuwapongeza tena Viongozi na Watendaji wa Wizara ya Vijana,Ajira na Uwekezaji kwa juhudi wanazochukua katika kutekeleza kazi zao pamoja na ushirikiano wao kwa Kamati hii. Vile vile, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha Hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa vile Kamati imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Sasa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako waijadili, watoe ushauri pamoja na mapendekezo yao na hatimae waiunge mkono Bajeti hii ili wamuwezeshe Mheshimiwa Waziri, Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba Kamati yangu naunga mkono hoja.

Naomba kuwasilisha.

………………………………………………………..........................

**(Mhe. Makame Mohammed Sufiani)**

**Mwenyekiti,**

**Kamati ya Uchumi na Uwekezaji,**

**Baraza la Wawakilishi,**

**<u>Zanzibar.</u>**